BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 07 Juni, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

153. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kuhakikisha nchi inakuwa na amani, ni jukumu la Serikali kuvitumia vyombo vyake vya ulinzi lakini pia kuwashirikisha wananchi katika kushirikiana na vyombo hivyo, ili nchi izidi kuwa na amani.

Je, kuna mikakati gani ambayo Serikali inaichukua juu ya kuwashirikisha raia kutoa taarifa za kiusalama na uhalifu.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

207. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Pamoja na kwamba yanafanyika kwa siri kubwa, lakini bado matumizi ya nishati ya kuni yanaendelea kushamiri yakiwemo maeneo ya Serikali kama ilivyo katika kiwanda cha mpira cha Mwane ndani ya jimbo la Pandani.

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha rasmi kampeni maalum kwa ajili ya upandaji wa miti ya pembezoni mwa fukwe na ya misitu Unguja na Pemba.

(b) Je, ni upi utaratibu wa ruhusa ya kukata miti na malipo yanayotozwa na Serikali kwa ruhusa hiyo.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kusimamia na kushajiisha kupatikana na kutumia nishati mbadala kwa bei nafuu kwa ajili ya matumizi ya majumbani na mabekari ili kupunguza ukataji wa miti kwa madhumuni hayo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

111. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Imekuwa jambo lililozoeleka na lisiloridhisha kwa wananchi wa Wilaya za Wete na Micheweni kurejeshwa bila ya kuhudumiwa wanapofuatilia vyeti vya kuzaliwa kwa kisingizio kwamba fomu zimeisha. Jambo hili linavunja moyo na linawapunguzia wananchi mapenzi na imani kwa Serikali yao.

(a) Je, Serikali inatumia utaratibu upi wa kupata fomu za vyeti vya kuzaliwa.

(b) Je, kwa nini fomu za vyeti vya kuzaliwa humalizika mara kwa mara katika Wilaya za Wete na Micheweni.

(c) Je, ni upi mkakati mpya na bora wa kuhakikisha kwamba fomu za vyeti vya kuzaliwa katika Wilaya za Wete na Micheweni zinapatikana bila ya kuadimika au kufichwa na watendaji wasio waaminifu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

184. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na ongezeko la safari za Unguja kwenda Pemba na kutoka Pemba kuja Unguja, lakini kwa muda mrefu huduma hiyo haitolewi kwa nyakati za usiku.

Je, Serikali haioni haja ya kurejesha safari za meli za abiria Unguja/Pemba na Pemba/Unguja kwa wakati wa usiku.

**Wizara ya Afya:**

212. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni jambo la kupongezwa kwa Serikali kwa kuzitumia vyema fedha zilizotokana na Akhueni ya Uviko 19 kutoka IMF na kuamua kuzijengea hospitali kubwa 11 za ghorofa katika kila Wilaya za Unguja na Pemba, ili kuleta huduma bora kwa wananchi. Hata hivyo, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba baadhi ya hospitali mpya hazina wafanyakazi wa kutosha, wakiwemo wauguzi na wakunga.

(a) Je, ni kwa nini katika hospitali hizi mpya, mfano Hospitali ya Micheweni, inatumia muuguzi mmoja kwa wodi mbili kwa wakati mmoja bila ya msaidizi wa muuguzi (Orderly).

(b) Je, baada ya ajira mpya, ni wauguzi na wasaidizi (Orderly) wangapi wamo katika hospitali na vituo vya afya vyote vya Unguja na Pemba.

(c) Je, kitakwimu, ni mapungufu yepi ya wafanyakazi katika hospitali na vituo vya afya vyote vya Unguja na Pemba ambayo Serikali inakabiliana nayo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

150. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Je, ni lini Wizara yako itafanya zoezi rasmi la kuondoa nguzo za umeme karibu na makaazi ya watu ambazo haziko katika mazingira salama.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali</u>:**

245. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Zanzibar imeanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na hivyo kuitegemea bahari, fukwe pamoja na mazao ya baharini katika maendeleo ya nchi pamoja na wananchi wake. Na kwa kuwa Sheria ya Uchumi wa Buluu ni ngeni katika masikio ya wananchi kwa hiyo taaluma kubwa inahitajika hususan kwa kizazi kipya.

Je, ni lini Serikali itarejesha mchipuo wa "Marine Sciences and Navigation" katika skuli zetu za sekondari kama ilivyokuwa skuli ya sekondari ya Lumumba katika miaka ya 70 na 90 ili kuzalisha wataalamu wa kutosha katika mambo ya uchumi wa buluu na bahari kwa ujumla.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

154. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Moja kati ya majukumu ya msingi ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ni kuhifadhi, kusimamia na kutunza mambo ya kale kwa dhamira ya kuyarithisha kwa vizazi vijavyo ili kuilinda historia ya Zanzibar.

Je, Wizara yako inachukua mikakati gani ya kuhakikisha kwamba hazina za kale hazipotei na zinaendelea kuwepo.

**III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>**

**<u>Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**07 Juni, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>**